

Mkate wa Siku

SIKU
30

NENO LA SIKU

Julai 2022

SIKU 01 - ZABURI 72:8a (SUV)

“Na awe na enzi toka bahari hata bahari...”

SIKU 02 - 1 YOHANA 5:14 (BHN)

“Na sisi tuko thabiti mbele ya Mungu kwani tuna hakika kwamba tukimwomba chochote kadiri ya matakwa yake, yeye hutusikiliza.”

SIKU 03 - KUMB. 11:12 (NEN)

“Ni nchi ambayo Bwana Mungu wenu anaitunza; macho ya Bwana Mungu wenu yanaitazama daima kutoka mwanzo wa mwaka hadi mwisho wa mwaka.”

SIKU 04 - ZABURI 33:12 (ONEN)

“Heri taifa ambalo Bwana ni Mungu wao, watu ambao aliwachagua kuwa urithi wake.!”

SIKU 05 - ISAYA 26:4 (SUV)

“Mtumainini BWANA siku zote Maana BWANA YEHOVA ni mwamba wa milele.”

SIKU 06 - KUTOKA 15:11 (BHN)

“Ewe Mwenyezi-Mungu, ni nani kati ya miungu anayelingana nawe? Ni nani aliye kama wewe uliye mtakatifu mkuu, utishaye kwa matendo matukufu, unayetenda mambo ya ajabu?”

SIKU 07 - 1 WATHESALONIKE 5:18 (NEN)

“shukuruni kwa kila jambo, kwa maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu kwa ajili yenu katika Kristo Yesu.”

SIKU 08 - YEREMIA 33:3 (SUV)

“Niite, nami nitakuitikia, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua.”

SIKU 09 - WAGALATIA 6:9 (BHN)

“Basi, tusichoke kutenda mema; maana tusipolegea tutavuna mavuno kwa wakati wake.”

SIKU 10 - ZABURI 19:14 (ONEN)

“Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu na Mkombozi wangu.”

SIKU 11 - ISAYA 55:8 (NEN)

“Kwa kuwa mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu,”

SIKU 12 - WARUMI 8:26b (SUV)

“...kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuomba kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.”

SIKU 13 - WAKOLOSAI 2:9 (BHN)

“Maana, ndani yake Kristo katika ubinadamu wake, umo ukamilifu wote wa Mungu.”

SIKU 14 - YOHANA 15:5b (ONEN)

“...Akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana, maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya jambo lolote.”

SIKU 15 - KUMB. 8:18a (NEN)

“Lakini kumbukeni Bwana Mungu wenu, ndiye ambaye huwapa uwezo wa kupata utajiri...”

SIKU 16 - ISAYA 46:4 (SUV)

“na hata uzee wenu mimi ndiye, na hata wakati wenu wa mvi nitawachukueni; nimefanya, nami nitachukua; naam, nitachukua na kuokoa.”

– ENDELEA UKURASA UNAOFUATA

SIKU 17 - YAKOBO 5:16 (SUV)

“Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.”

SIKU 18 - ZABURI 61:2b (SUV)

“Uniongoze juu ya mwamba nisioweza kuupanda.”

SIKU 19 - MAOMBOLEZO 3:22 (BHN)

“Kwamba fadhili za Mwenyezi-Mungu hazikomi, huruma zake hazina mwisho.”

SIKU 20 - MATHAYO 5:3 (ONEN)

“Heri walio maskini wa roho, maana Ufalme wa Mbinguni ni wao.”

SIKU 21 - ISAYA 41:13 (NEN)

“Kwa maana Mimi ndimi Bwana, Mungu wako, nikushikaye mkono wako wa kuume na kukuambia, Usiwe na hofu, nitakusaidia.”

SIKU 22 - WAEBRANIA 4:16 (SUV)

“Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.”

SIKU 23 - NEHEMIA 9:10b (BHN)

“Ukajipatia umaarufu uliopo mpaka leo.”

SIKU 24 - ZABURI 90:14 (NEN)

“Tushibishe asubuhi kwa upendo wako usiokoma, ili tuweze kuimba kwa shangwe na kufurahi siku zetu zote.”

SIKU 25 - MITHALI 16:20b (ONEN)

“...tena amebarikiwa yeye anayemtumaini Bwana.”

SIKU 26 - ISAYA 50:4 (SUV)

“Bwana MUNGU amenipa ulimi wa hao wafundishwao, nipate kujua jinsi ya kumtegemeza kwa maneno yeye aliyechoka,...

SIKU 27 - WAEFESO 1:8 (BHN)

“aliyotukirimia bila kipimo! Kwa hekima na ujuzi wake wote.”

SIKU 28 - LUKA 1:37 (NEN)

“Kwa maana kwa Mungu hakuna lisilowezezana.”

SIKU 29 - 2 NYAKATI 20:15b (SUV)

“...BWANA awaambia hivi, Msiogope, wala msifadhaike kwa ajili ya jeshi kubwa hili; kwani vita si yenu bali ni ya Mungu.”

SIKU 30 - ZABURI 5:8a (ONEN)

“Niongoze katika haki yako, Ee Bwana...”

SIKU 31 - ISAYA 66:13a (BHN)

“Kama mama amtulizavyo mwanawe, kadhalika nami nitawatuliza;”

Makala hii imechukuliwa
kutoka
www.biblesociety.ca © Haki
zote zimeifadhiwa.

*Tunawashukuru sana kwa kuungana
na sisi kuenza Neno la Mungu hapa
Tanzania na duniani kote kwa ujumla.*

Chama cha Biblia cha Tanzania
16 Hatibu / 9 Barabara, Eneo la Madukani,
S.L.P 175, Dodoma - Tanzania

<https://shop.biblesociety-tanzania.org/>
<https://tanzanian.bible/>
<https://biblesociety-tanzania.org>

CHAMA CHA BIBLIA
CHA TANZANIA

&



Canadian
Bible Society

10 CARNFORTH ROAD, TORONTO, ON M4A 2S4
TOLL FREE: 1.800.465.2425 EMAIL: INFO@BIBLESOCIETY.CA
WWW.BIBLESOCIETY.CA